

Majina Fiche ya Asili Wanayopewa Watu na Uchanuzi wake wa maana katika Lugha na Semi za Kiswahili

Sauda Uba Juma

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

Ikisiri

Azma ya makala haya ni kuonesha jinsi majina majina ya asili yenye maanafiche wanayopewa watu yanavyochanuzwa maana tofauti katika lugha ya Kiswahili. Watu wa jamii mbalimbali wana desturi ya kuwapa watoto wao majina yenye maana iliyojificha kwa malengo maalumu. Malengo hayo yanaweza kutokana na mazingira au vigezo mbalimbali vinavyosababisha watu wa jamii zingine kuwapa watoto wao majina ya namna hiyo. Pamoja na ukweli huo, bado baadhi ya watu hawajaelewa sawasawa maana ya majina hayo katika Kiswahili. Hivyo basi katika makala haya tumejikita zaidi na kuangazia majina hayo yanatoa maana gani katika lugha ya Kiswahili na jinsi maana hizo zinavyoakisi semi mbalimbali za Kiswahili. Data za makala haya zilikusanywa uwandani kwa kutumia mbinu za hojaji, usaili, mahojiano, udusuru wa nyaraka mbalimbali pamoja na kamusi ili kuapata maana ya majina hayo. Aidha, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wake, ulitumia njia ya kitaamuli na wakati mwingine data zilichambuliwa kitakwimu. Zaidi ya hayo nadharia ya semiotiki ilitumika kuogoa uchanganuzi wa data za makala haya.

Maneno Muhimu: *Majina Fiche, Lugha, Semi, Kiswahili, Asili, Watu*

Utangulizi

Utoaji wa majina ya watu ni utaratibu uliojengeka dunia kote tangu azali. Mtoto anapozaliwa ni lazima apewe jina fulani. Majina yanayotolewa mara tu pale watoto wanapozaliwa, au mara nyingine kwa baadhi ya jamii mtoto anapozaliwa anakaa baada ya siku saba ndipo anapewa jina. Majina yanayotolewa yana taratibu zake kutegemeana na jamii husika. Wapo wanaotoa majina kulingana na koo zao, wengine wanajikita kulingana na sifa za vitu au watu wenye hadhi ya juu. Pia wapo wanaowapa watoto wao majina kulingana na mazingira au vigezo mbalimbali vinavyotumika katika utoaji wa majina ya kike na kiume katika jamii ya zao (Ali 2016). Hivyo kama tulivyoeleza hapo awali kuwa makala haya yamejikita zaidi kuchunguza majina ya asili yenye maana fiche wanayopewa watu katika maeneo mahususi kisiwani Pemba na jinsi yanavyotoa maana katika lugha ya Kiswahili na semi zake. Suala hili la utoaji wa majina, limewahi kuchunguzwa na wanazuoni mbalimbali ambao wamefanya utafiti kuhusu majina wanayopewa watu katika jamii kadhaa ulimwenguni. Wanazuoni hao wamebaini mambo tofauti yanayohusiana na utowaji na upewaji wa majina katika jamii walizotafiti. Mathalani, Omary (1970) anadai kuwa jamii ya Chasu watu wanapewa majina kutokana na vigezo vya mtagusano wao wa kijamii na jamii za kigeni. Kadhalika kigezo cha hali au sura ya nchi na matukio kadha wa kadha yanayotokea katika jamii zao. Naye Braver (1979) anadai kuwa mtu mmoja katika jamii ya Wachina anaweza kupewa majina mengi tofauti kulingana na nyakati tofauti ambazo anapitia katika kipindi chote cha maisha yake. Vilevile Chulk (1992) alifanya utafiti kuhusu majina ya watu wa Najeria ambapo alibaini kuwa, kwa kawaida watu wanapewa majina kutokana na matukio fulani, vitu vikubwa vya kushangaza, siku, au wiki ambayo mtu huyo amezaliwa.

Agyekum (2006) kwa upande wake naye anabaini kuwa watu wa kabila la Akan wanawapa watoto wao majina kulingana na siku wanazozaliwa. Mara nyingi huwa ni majina yanayotokana na ukoo katika familia zao mbalimbali. Baitan (2010) naye anabainisha kuwa majina katika jamii ya Kihaya yanatokana na matukio mbalimbali katika jamii kama vile itikadi na mambo mengine yanayohusiana na itikadi hizo. Manyasa (2010) naye alifanya utafiti katika jamii ya Wasukuma (2010) ambapo alieleza kuwa majina ya watu katika jamii hiyo, aghalabu yanatokana na matukio aliyopambana nayo

mtoto akiwa katika tumbo la mama yake kabla hajazaliwa. Matukio hayo yanaweza kuwa magonjwa makali endapo yatampata mtoto huyo wakati anapozaliwa.

Kwa ujumla wataalamu mbalimbali waliofanya utafiti katika uga huu wanabainisha kuwa kuna mitazamo tofauti inayotumika katika utoaji wa majina ya watu katika jamii nyingi ulimwenguni. Kwa mfano James (2011) anabainisha mitazamo mikuu miwili ambayo ni mtazamo wa kimaana na mtazamo wa kimatilaba. Mitazamo hii aliibaini wakati alipofanya utafiti wa majina ya watu wa kabila la Lulogooli. Kwa ufupi baadhi ya tafiti tangulizi, zinabainisha kwamba kuna mazingira, matukio na vigezo tofautitofauti vinavyoweza kutumika katika utoaji wa majina ya kike na kiume katika kila jamii duniani. Hivyo si lengo la makala haya kujikita katika vigezo hivyo vilivyobainishwa, isipokuwa vigezo hivyo vimetajwa tu pale ilipolazimika kufanya hivyo kwa minajili ya kutolea ufafanuzi zaidi. Makala haya yamegawika katika sehemu zifuatazo: utangulizi, mwega wa kinadharia, methodology, matokeo ya utafiti na hitimisho na mapendekezo.

Mwega wa Kinadharia

Makala haya yameongozwa yameongozwa na Nadharia ya Ujinaishaji ambayo iliasisiwa na wanafalsafa wa kimapokeo kama vile Plato, Aristototele, Protagoras, Thrax na wengineo. Wanafalsaa hao walizaliwa miaka 300 na zaidi kabla ya kristo ambao walichunguza lugha za Kigiriki na Kilatini katika viwango mbalimbali. Viwango hivyo vilianza katika kategoria za nomino katika uchambuzi wake wa sentensi ambapo sentensi iligawanywa katika sehemu mbili tu nazo ni nomino na kitenzi. Baadaye kadri muda ulivyosonga uchunguzi wao ulibaini kategoria nyingine kama vile kibainishi, kiunganishi, kielezi na kategoria nyinginezo. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kwamba, lugha huwa na safu mbili ambazo ni kiashiria na kiashiriwa. Jambo muhimu la msingi hapo ilikuwa ni kukipa kila jina lake. Kwa msingi huo basi, kiashiria kilichukuliwa kwamba ni neno katika lugha ambalo linarejelea kitu halisi ambacho ni kiashiriwa. Hivyo, viashiria ni maneno au ishara ambavyo hurejelea vitu halisi katika jamii.

Lugha yoyote ile iwayo ulimwenguni kote, huwa na majina ya pekee ambayo yanarejelea watu, siku za wiki, miezi, mito, maziwa, watu mashuhuri, miji, vijiji na kadhalika. MATHALANI, Mwinyi, Dar es Salaam, Ijumaa. Desemba na mengineyo mengi. Hata hivyo, ni muhimu kusisitiza hapa kuwa majina yanayotolewa mara nyingi huwa hayana uhusiano wa moja kwa moja na kirejelewa chake. Uhusiano wake mara nyingi unakuwa wa kinasibu tu, ingawa baadhi ya jamii tangu kale hadi sasa uhusiano wa kiashiria na kiashiriwa unajitokeza moja kwa moja. Nadharia hii ni muhimu sana kwani hata mtoto au mtu yeyote anapojifunza lugha hawezi kukwepa kutumia mbinu ya ujinaishaji. Aidha, nadharia hii inashadidiwa hata kwenye vitabu na imani za kidini husani dini ya Kiisilamu na Kikiristo. Tunaelezwa kwamba baada ya Mwenyezi Mungu kuumba ulimwengu na vitu vyote vilivyomo ndani yake, alimpa Adamu jukumu kubwa la kukipa kila kitu ulimwenguni jina lake.

Nadharia ya Ujinaishaji pamoja na umuhimu wake katika kila lugha, ilionekana kuwa na udhaifu kwa kuwa mosi, si kila kitu kilichopo kinaweza kurejelewa kwa jina. Kwa mfano matukio mbalimbali, hali, dhana na vitu vyote vinavyohusiana. Pili nadharia hii, inasisitiza zaidi nomino na kupuuza aina nyingine za maneno kama vile: vitenzi, vielezi, vivumishi, vihisishi na kadhalika. Tatu, kila lugha ina njia yake ya kipekee ya kuvipa vitu au hali majina. Hivyo, kutokana na upekee wake huo ni dhahiri kuwa majina ya vitu au hali hizo zinaweza kutofautiana kutoka lugha moja hadi lugha nyingine. Tukiachia mbali udhaifu huo, nadharia hii ni muhimu na imefanikiwa kwa kiasi fulani, kwa kuwa kuvipa vitu majina ni hatua mujarabu katika kila lugha. Nadharia ya ujinaishaji, imeshabihiana na nadharia nyingine kama vile Nadharia ya Simiotiki, Nadharia ya Urejeleo na Nadharia ya Giles (1979). Hivyo basi, katika makala haya Nadharia ya Ujinaishaji imekifu na kusadifu barabara katika uchambuzi wake wa data kwa kuwa tumejiegasha zaidi na majina ya asili yenye maana fiche yanayotoa maana tofauti katika lugha ya Kiswahili na semi zake.

Methodolojia

Data za makala haya zilikusanywa katika vyanzo mbalimbali kuhusu majina ya asili yenye maana fiche yanavyotoa maana katika lugha ya Kiswahili. Kwa ujumla njia nne zilitumika katika kukusanya data. Mbinu ya kwanza iliyotumika ni ile ya uwandani ambapo data zilikusanywa katika kisiwa cha Pemba. Vijiji ambavyo vilihusishwa katika utafiti huu ni Kisiwa Panza na Makoongwe vilivyoko katika mkoa wa Kusini Pemba. Aidha, kwa upande wa mkoa wa Kaskazini Pemba, data zilikusanywa Kiuyu Minungwini na Ole. Uchaguzi wa sehemu hizi, haukufanywa tu kinasibu bali ulihusisha utafiti wa awali aliofanya mtafiti pamoja na wasaidizi wake. Kwa mujibu wa utafiti huo, ilibainika kwamba maeneo hayo ndiyo yanayoongoza zaidi kwa wanajamii kuwapa watoto wao majina ya namna hiyo. Hii inatokana na tafiti za awali zilizofanywa na kugudulika kwamba watu wa maeneo hayo bado hawajathiriwa sana na wageni kama Waarabu, Waingereza na Washirazi (Juma, 2011; 2019). Kwa mnasaba huo, huenda ndiyo maana hadi leo bado baadhi yao, wanaendelea kuwapa watoto wao majina yao ya kiasili.

Mbinu ya pili iliyotumiwa ni usaili ambapo mtafiti alionana ana kwa ana na wenyeji 10 katika kila eneo. Kati ya watu hao 10, kila eneo lilijumuisha wanawake 5 na wanaume 5 ambapo jumla ya watu 40 walimpatia mtafiti data za kutosha. Lengo la kufanya hivyo lilikuwa kupata mawazo yao kuhusu aina ya majina ya majina ya asili yenye maana funge wanayowapa watoto wao katika jamii zao. Mbinu hii ilitumia usampulishaji lengwa kwa minajili ya kuwapata watu hao ambao walitupatia taarifa tulizozihitaji. Sababu kubwa iliyotumika kuwapata watoataarifa hao, ilikuwa ni uwezo na weledi wao wa kufahamu mambo mbalimbali ya kihistoria na kijamii. Aidha, watoataarifa hao walichaguliwa kutokana na umahiri wao katika lahaja yao pamoja na umahiri walionao katika lugha ya Kiswahili.

Mbinu ya tatu ilijumuisha mahojiano ya vikundilengwa ilitumika kwa minajili ya kupata taarifa mbalimbali zinazohusiana na utafiti wa makala haya. Majadiliano yalikusishwa watu ambao tayari wameonesha uelewa na mapenzi yao ya dhati kabisa kuwa sehemu ya watoataarifa kupitia ushiriki wao katika mbinu ya usaili. Mbinu hii ilitusaidia kuthibitisha data ambazo zimeshakusanywa kwa mbinu nyingine kabla ya uchambuzi ambayo ni usaili. Katika kuitumia mbinu hii tulijadiliana na wazee kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na utoaji wa majina ya watoto wao katika jamii zao. Aidha, mtafiti alilazimika kutumia kinasasauti kurekodi mazungumzo mbalimbali yaliyojadiliwa katika vikundi vilikavyohusika. Kinasasauti kilitumika pamoja na zana zingine kama vile kinyonyi na simu kwa ajili ya kuhifadhi data za kidijiti. Mwisho komputa ilitumika kama kifaa cha kusikilizia mazungumzo yaliyorekodiwa na kuhifadhiwa kwenye kinyonyi na kuandikia maelezo ya uchambuzi wa data za makala haya.

Mbinu ya nne iliyotumika katika ukusanyaji wa data za makala haya, ni ile iliyohusisha upitiaji wa nyaraka mbalimbali zinazoonesha maana ya majina hayo tuliyoyakusanya kutoka uwandani. Machapisho hayo yalijumuisha kamusi mbalimbali za Kiswahili sanifu (2004) na Kiswahili Fasaha (2010) ili kupata maana mbalimbali. Vilevile, mbinu hii ya upitiaji wa nyaraka, ilitumika ili kuhakiki maana za majina zilizopatikana kupitia mbinu zingine zilizotumika uwandani kama zilivyobainishwa katika makala haya.

Mbinu ya Uchambuzi wa Data

Utafiti huu ulitumia mkabala mseto katika kuchambua data. Mkabala huu unazingatia uchambuzi wa data zinazowasilishwa kwa njia za maelezo (kitaamuli) na zile ambazo zinawasilishwa kwa kutumia taratibu za kitakwimu. Mkabala wa kitaamuli katika uchambuzi wa makala haya ulitumia mbinu za kimaelezo na kiufafanuzi katika kutafuta maana fiche zilizomo katika majina mbalimbali ya asili yaliyotafitiwa na kubainishwa. Kwa upande wa mkabala wa kitakwimu, kimsingi ulijikita katika uchambuzi wa data kitakwimu, kuonesha idadi ya majina yaliyomo katika kundi fulani. kwa kutumia namba.

Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa msingi wa makundi mbalimbali ya majina kulingana na maana zinazopatikana katika kila kundi. Makundi hayo ni: Majina ya mafumbo, maombi, uvumilivu, mafanikio, kukweza, kutwesa, kutweza pamoja na siku za wiki.

Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotokana na Mafumbo

Majina haya yanatokana na semi mbalimbali za Kiswahili ambayo yanatolewa kimapumbo. Kwa mujibu wa watoataarifa walieleza kwamba, huo ndiyo ulikuwa utaratibu wao tangu azali ambao nao waliurithi. kutoka kwa wazee wao. Lengo hasa la wazee kuwapa watoto wao wajina ya namna hiyo lilikuwa ni ama kutaka kumfumba au kumsema mtu bila mwenyewe kujua au kumuonya mtu na kumkemea. Tuchunguze mifano katika Jedwali lifuatalo.

Jedwali Na.1: Majina Fiche Yanayotokana na Mafumbo

Na.	Jina	Maana katika Kiswahili Sanifu
1.	Andikalo	Analoandika
2.	Hafunzwa	Hafundishwi
3.	Hakupukwa	Hakurupuki
4.	Haurambiki	Hauwezi kurambika
5.	Ndiye	Ndiye
6.	Mwajipiani	Munaringiya nini
7.	Ngayani	Nipeni na mimi
8.	Ntaisha	Mtayamaliza
9.	Simapya	Mambo ya kawaida tu sio mapya (mageni)
10..	Semeni	Endeleeni kusema

Chanzo: Data ya Uwandani (2023)

Mifano ya majina yaliyomo katika Jedwali Na.1 hapo juu yanaonekana kutokana na mafumbo au semi mbalimbali za Kiswahili. Katika lugha ya Kiswahili kuna methali mbalimbali ambazo zinatumiwa kutoa mafunzo, kuonya, kukosoa ama kuitahadharisha jamii. Kwa hakika katika jamii yoyote iwayo, kuna masahibu kadhaa wa kadhaa ambayo yanaweza kuikumba jamii hiyo juu ya masuala hayo. Hivyo, semi kama hizo zinatumiwa ili kuchukua nafasi hiyo. Jamii ya Wapemba nao wanazitumia semi hizo kupitia lahaja yao ya Kipemba, kwa mwamvuli wa majina wanayowapa watoto wao. Kwa mfano:

Jina	Methali ya Kiswahili	Tafsiri ya Kiswahili
Andikalo	Aandikalo Mungu halifutiki	Analoandika Mungu halifutiki
Hafunzwa	Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu	Asiyefundishwa na mamake atafundishwa na ulimwengu
Hakupukwa	Mwanadamu hakupukwa	Mwanadamu hakurupuki tu
Haurambiki	Hauliki wala haurambiki	Haiwezekani kuula wala kuuramba
Ndiye	Usemaye ndiye kumbe siye	Unayedhani ndiye anaweza kuwa siye yeye ni mwengine
Mwajipiani	Mwajipa bure hamuna mulilonalo	Munaringa bure hamuna kitu chochote
Ngayani	Chwichwi gawana na mwenzio	Kidogokidogo mgawie na mwenzako
Ntaisha	Hata mufanyeje hamuyeshi	Hata mukifanya nini hamuwezi kuyamaliza
Simapya	Simapya yayo kwa yayo maji ya futi na nyayo	Yaleyale ya kawaida hakuna mapya
Semeni	Mtasema mchana usiku mutalala	Mutasema mchana usiku mtalala

Tukichunguza mifano hiyo ya majina ya watu inadhihirisha kwamba inatokana na semi mbalimbali za Kiswahili, kama ambavyo tumeelezwa na baadhi ya watoataarifa tuliowahoji. Majina hayo yalitolewa kimapumbo ili kuficha kile ambacho kinamkera na kumsokota mtu katika nafsi yake. Majina hayo 6 kati ya 10 wanapewa watoto wa kike ambayo ni *Hafunzwa*, *Hakupukwa*, *Ndiye*, *Mwajipiani*, *Ngayani* na *Semeni*. Majina 3 katika 10 wanapewa watoto wa kiume: *Haurambiki*, *Ntaisha* na *Simapya*. Jina 1 kati ya 10 ambalo ni *Andikalo* wanapewa watoto wa jinsia zote, wanawake na wanaume.

Majina yenye Maana Fiche Yanayotokana na Maombi

Haya ni majina ambayo yanabeba hisia fulani za kimaombi kutokana na mambo yanayomthakili mtu. Kwa kawaida binadamu tupokosea au tunapokuwa na matatizo ya muda mrefu, tunatakiwa tumrudie Mwenyezi Mungu kwa maombi. Watu wa Pemba wanajikurubisha sana kwa Mwenyezi Mungu wao kwa kuomba msaada wa utatuzi wa matatizo yao yanayowasibu. Jamii ya watu wa Pemba walio wengi, wana imani na dini ya Kiisilamu, kwa mnasaba huo kila wanapopatwa na shida wanakuwa wepesi kumuomba Mwenyezi Mungu, wakiamini kuwa ndiye pekee anayeweza kuwatatulia shida zao. Jambo hili pia linajidhihirisha kupitia baadhi ya majina wanayowapa watoto wao. Tutalii mifano iliyomo katika Jedwali Na. 2 hapo chini.

Jedwali Na.2: Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotokana na Maombi

Na.	Jina	Maana katika Kiswahili Sanifu
1.	Hukumu	Kitendo cha mtu kama vile hakimku kukata shauri juu ya jambo kwa mujibu wa taratibu za kisheria zilizowekwa ¹
2.	Jaala	Mambo mtu afanyayo kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu (Majaaliwa)
3.	Nusura	Kusalimika na hatari yoyote iliyotaka kumfika mtu.
4.	Nshibe	Kutosheka na jambo fulani
5.	Npaji	Mtoaji
6.	Rahimu	Jina linalotumika kumtaja Mwenyezi Mungu linaloashiria rehema zake ²
7.	Riziki	Neema anayoipata kiumbe kutokana na uwezo wa Mwenyezi Mungu.
8.	Takidiri	Uwezo wa Mwenyezi Mungu juu ya matukio ya mambo kwa viumbe.
9.	Tupe	Maombi ya waja kwa Mola wao
10.	Wastara	Viumbe wenye kuhifadhiwa na Mwenyezi Mungu

Chanzo: Data ya Uwandani (2023)

Utafiti umebaini kuwa majina yote hayo yaliyomo kwenye Jedwali Na. 2 hapo juu ambayo wanapewa watoto, yanalenga kumuomba Mwenyezi Mungu kama tulivyokwishabainisha hapo kabla. Maana ya majina hayo pia yanakwenda sanjari na methali mbalimbali za Kiswahili zenye muelekeo wa kuomba msaada kwa Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

¹ Tafsiri ya BAKIZA (2010: 120)

² Tasiri ya Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004: 345)

Jina	Methali za Kiswahili	Tafsiri ya Kiswahili Sanifu
Hukumu	Hukumu ni yake Mungu	Mwenyezi Mungu ndiye anayeweza kulipa kutokana na uovu wowote anaofanyiwa mtu
Jaala	Mola nijaaliye nipate change na miye	Maombi ya mtu kwa Mola wake ili na yeye aweze kumiliki cha kwake
Nusura	Mola tunusuru kwa kila jambo	Mola ndiye mwenye uwezo wa mwisho wa kumkinga mtu na tatizo lolote
Nshibe	Nshibe Muumba wako	Tatizo lolote linalompata binadamu mshitakiye Mungu, Yeye ndiye mtatuzi wa kila jambo
Npaji	Mpaji ni Muungu	Mwenyezi Mungu ndiye anayetoa kila jambo
Hahimu	Mwenyezi Mungu ndiye hakimu Muadilifu	Rehema zote zinatokana na Mwenyezi Mungu
Riziki	Riziki mafungu saba	Mwenyezi Mungu ndiye anayegawa riziki kwa kila kiumbe chake kilichopo duniani (Hakuna mja anayekosa riziki)
Takidiri	Takidiri Lghazizi	Mwenyezi Mungu akitaka jambo liwe linakuwa tu, hakuna wa kulizua.
Tupe	Mola tupe kila lenye khaeri	Kuomba jambo jema kwa Mwenyezi Mungu
Wastara	Wastara hasumbuki	Mwenye kusitiriwa na Mungu hababaishwi na chochote

Majina hayo yanayotokana na maombi yanasadifu barabara jamiii tunayoizungumzia. Takribani yote yameegemea upande wa dini ya Kiislamu ili kumuomba Mwenyezi Mungu katika shida zao tofautitofauti. Utafiti wa Ali pia umedhihirisha jambo hili kama anasemavyo:

.....kwa vile watu wengi wa jamii ya Kipemba itikadi yao ya kidini ni ya kiislamu, majina mengi yameathiriwa na itikadi ya dini hiyo. Hivyo Wapemba hutumia majina yanayopatikana katika kitabu cha Kur-ani ambayo ni majina yanayoelezea historia za wajumbe wa Mwenyezi Mungu waliotumwa kwa wanaadamu, wajumbe hao wote walikuwa ni wanaume (Ali 2016: 68)

Kwa mujibu ya watoataarifa majina yanayoingia katika kundi hilo, mengi yalitolewa kwa maombi mahususi. Maombi hayo ni kuomba mtoto kwa ambaye hajajaaliwa kupata mtoto kwa mfano jina *Jaala*. Aidha, wakati mwingi majina hayo yalitolewa kwa kumuomba Mwenyezi Mungu amueke mtoto ambaye amezaliwa, kwa kuwa wengine wote waliozaliwa walifariki mathalani jina *Tupe*. Majina mengine kama vile; *Nshibe, Nusura, Npaji, Hahimu Riziki, Takidiri* na *Wastara* yalitolewa kwa ajili ya kumuomba Mwenyezi Mungu kwa minajili ya kuwatatulia kadhia zao zinazowatanza.

Halikadhalika, majina yote ya mkondo huo wa dini ya Kiislamu, tumegundua kwamba yameakisi maana ya semi mbalimbali zilizomo katika lugha ya Kiswahili kama ilivyokwishabainishwa. Tulijaribu kuwadadisi watoataarifa kuhusu majina hayo walitueleza kwamba, majina hayo yapo yanayotolewa kwa wanawake peke yake, wanaume peke yake na mengine yanatolewa kwa wanaume na wanawake. Tulipozidi kuwadodosa sababu ya majina mengine yanatolewa kwan pande zote mbili yaani wanawake na wanaume walikosa majibu na kudai ndiyo walivyozoea. Hivyo, majina 3 kati ya 10 ambayo ni *Npaji, Tupe* na *Wastara* yanatolewa kwa ajili ya watoto wa kike wakati majina 4 kati ya 10 *Hukumu, Jaala, Hahimu na Takidiri* yanatolewa kwa ajili ya wanaume tu. Vilevile, majina 3 kati ya 10, *Nshibe, Nusura* na *Riziki* yanatolewa kwa ajili ya watoto wa kike na kiume.

Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotokana na Matukio

Uchunguzi wetu umebaini kuwa katika jamii ya Wapemba, kuna majina ya asili yenye maana fiche, yatokanayo na matukio au misimu tofauti katika jamii. Madai haya yameungwa mkono na watafiti wengine ambao waliwahi kufanya uchunguzi wa masuala haya katika jamii zao mbalimbali. Mathalani, Chulk (1992) alichunguza majina ya watu wa Naijeria ambapo alibainisha kuwa, kwa kawaida watu wa jamii hiyo wanapewa majina kutokana na matukio fulani au vitu vikubwa vya kushangaza. Aidha, imebainika kuwa majina ya watu katika jamii mbalimbali kama vile jamii ya

Wasukuma, yametokana na matukio yaliyotokea kipindi cha kuzaliwa mtoto na magonjwa makali yanayompata mtoto kipindi cha kuzaliwa. Kwa mfano *Mboku* jina ambalo hupewa mtoto mwenye uoni hafifu Manyasa (2010). Tuangalie mifano ifuatayo ambayo inaonesha majina ya asili yenye maana fiche yanayotokana na matukio mbalimbali.

Jedwali Na. 3: Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotokana na Matukio

Na.	Jina	Maana katika Kiswahili Sanifu
1.	Bei	Kiasi cha fedha kinachotumika kununulia au kuuzia kitu
2.	Karume	Raisi wa kwanza wa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, iliyopatikana baada ya kupinduliwa serikali ya Kisultani
3.	Bie	Aina fulani ya chakula mfano wa magimbi.
4.	Mapinduzi	Kuondolewa madarakani viongozi wa serikali
5.	Mwasada	Njaa kali ambayo inatokea katika jamii ambapo watu wanakosa chakula kwa muda mrefu
6.	Voti	Kupiga kura

Chanzo: Data ya Uwandani (2023)

Kama ambavyo tumenainisha katika tafiti tangulizi kwamba, baadhi ya majina wanayopewa watu yanatokana na vigezo na matukio mbalimbali yanayoikumba jamii fulani. Imethibitishwa kwamba Wapemba nao wametumia kigezo hicho kuwapa watoto wao baadhi ya majina ya asili yenye maana fiche. Lengo la kutoa majina hayo ni kuakisi jambo au hali fulani ya maisha waliyonayo kwa kipindi hicho. Yapo majina katika kundi hili ambayo yana maana ilinayowakilisha jambo au hali iliyo dhahiri. Kwa mfano: *Bei*, *Karume* na *Mapinduzi*, majina yote hayo yanajidhihirisha kimaana kutokana na matukio muhimu ya kiserikali yaliyotokea kuanzia miaka ya 60 na kuendelea. Ama kwa upande wa jina la *Bei* kwa mujibu wa watoataarifa liliibuliwa rasmi kipindi cha kubanda kwa bei ya vyakula na mahitaji muhimu ya kijamii katika miaka hiyo. Majina yote hayo, wanapewa watoto wenye jinsia ya kike.

Fauka wa hayo, tukichunguza Jedwali Na. 3 hapo juu tunabaini majina yenye maana iliyojificha katika lugha ya Kiswahili. Tunadiriki kusema hivyo kwa kuwa maana zake zote zimegubikwa kutokana na matumizi ya lugha ya jamii yao. Masanjila na wenzake waliwahi kuyasema haya:

Kwa kuwa jina hutokana na lugha ya jamii, jina hilo hubeba maana inayotokana na utamaduni na mazingira ya jamii hiyo. Majina haya ya familia hubeba maana mbali mbali ambazo kimsingi hueleweka na wanajamii wenyewe kutokana na maarifa, elimu na utamaduni unaofanana. Msanjila na wenzake (2010: 52-53).

Kwa upande mwingine, jina *Bie* lilitokana na aina fulani ya chakula chenye kuwasha sana. Chakula hicho ambacho kinafanana na magimbi kililiwa sana kipindi cha mwaka 72 ambapo tulielezwa kwamba kihistoria, kilikuwa ni kipindi cha njaa kali nchi kote Tanzania. Jina hili walipewa watoto wa kiume. Vilevile, jina *Mwasada* lina maana ya njaa kali wakati jina *Voti* lina maana ya kupiga kura. Majina yote hayo, wanapewa watoto wenye jinsia ya kike. Hata hivyo, ingawa majina hayo ni ya kiasili hayaonekani kuakisi semi za Kiswahili kwa kuwa yamejikita zaidi katika matukio mbalimbali.

Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotokana na Uvumilivu

Tukiachilia mbali majina yanayotokana na matukio au hali fulani, kupitia mbinu ya mahojiano utafiti huu umebaini kuwapo kwa majina ya asili yatokanayo na uvumilivu. Uvumilivu huo, unatokana na masahibu pamoja na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika ndoa zao au jamii zao. Ndipo pale majina ya namna hiyo yalipoibuka. Baadhi ya wanajamii wanayatumia majina haya, kwa kujipa moyo wa ushindi endapo watayavumila mateso su matatizo hayo wanayokumbana nayo. Hebu tuchunguze mifano katika Jedwali Na. 4 kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 4: Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotokana na Uvumilivu

Na.	Jina	Maana katika Kiswahili Sanifu
1.	Safinia	Safisha nia
2.	Shida	Matatizo (dhiki)
3.	Subira	Stahamala
4.	Tabu	Matatizo

Chanzo: Data ya Uwandani (2023)

Kwa mujibu wa watoataarifa, majina hayo yalishamiri sana hapo zamani ikilinganishwa na kipindi cha sasa hivi kama anavyosimulia mama mmoja:

Magina ja haya tweekiwapa wenetu kama silaha ya kupunguza mavune ya machugu. Hata ndoa zetu zikidumu, dulfu lalamina, ha njoo uchunze leo watu wamaowana unju majakukyani wamaachana maana hawana stahamala. Sasa wataka magina yao ya kukohoa tu, mpaka uyatile rohoni ndiyo ulitanke.

Majina kama haya tulikuwa tukiwapa watoto wetu kwa ajili ya kupunguza maumivu. Hata ndoa zetu zilikuwa zikidumu milele, sasa ngalia leo watu wanaoana asubuhi jioni wanaacha kwa kuwa hawawezi kustahamili. Sasa wanataka majina magumu ambayo mpaka yatamkiwe kwenye koo (Tafsiri yangu)

Majina hayo yalitumika bega kwa bega pamoja na semi mbalimbali za Kiswahili ambazo zinaifundisha jamii jinsi ya kuvumilia na kutatua matatizo yanayowasibu kwa njia ya amani. Mifano ifuatyo inadhahirisha jambo hilo.

Jina	Methali	Tafsiri ya Kiswahili Sanifu
Safinia	Nia safi hushinda kafara	Nia safi (roho) haishindwi na chochote hata kafara haisaidii
Shida/Tabu	Shida/Tabu za dunia zinamwishowe	Kila tatizo lina ukomo wake wa kumalizika
Subira	Mwenye kusubiri hajuti/subira yavuta kheri	Siku zote mwenye kusubiri au kuvumilia atafanikiwa

Kijumla, majina *Shida*, *Tabu* na *Subira* yanatumika kwa jinsi zote, wanawake na wanaume ambapo jina *Safinia* linatumika kwa jinsi ya kike pekee.

Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotumika kwa Ajili ya Kumkweza Mtu

Majina haya mara nyingi yanatokana na urithi kwenye familia husika. Kwa kawaida mtu anaweza kumpa mtoto wake jina la mama yake mzazi, baba yake mzazi au mama yake mdogo. Lengo hasa ni kumtukuza au kumpa heshima mzazi wake. Tufuatile mifano katika Jedwali Na. 5 hapo chini:

Jedwali Na. 5: Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotumika kwa Ajili ya Kumkweza Mtu

Na.	Jina	Maana katika Kiswahili Sanifu
1.	Bimdogo	Lakabu ya hishima ya ndugu wanawake ³
2.	Bimkubwa	Lakabu ya mama mzazi au mwanamke mwenye kuhishimika ⁴
3.	Mbwana	Jina linalotumika kumtukuza baba mzazi (bwana)
4.	Shaibu	Mwanamme mwenye umri mkubwa sana ⁵

Chanzo: Data ya Uwandani (2023)

Kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 5 hapo juu, majina yote hayo yanatumika kurejelea heshima kwa wazazi wote wawili. Wazazi ambao ni bibi au babu wote wanakuwa na majina yao

³ Kamusi la Kiswahili Fasaha (2010: 27)

⁴ Kamusi la Kiswahili Fasaha (2010: 27)

⁵ Kamusi la Kiswahili Fasaha (2010: 360)

halisi ambayo walipewa na wazazi wao. Hata hivyo, majina hayo halisi hayatumiki kuwaita wajukuu waliozaliwa na badala yake, yanatumika majina hayo ili kuonesha heshima ya hali ya juu kwa wazazi wao. Tulipojadiliana na watoataarifa kuhusu suala hili walidai kuwa, kuwaita watoto wao majina halisi ya wazazi wao inaonesha kumdharau mzazi. Wanaamini kuwa watoto kwa kawaida huwa wanafanya makosa mbalimbali, hivyo kuwaita kwa majina halisi ya wazazi ni sawa na kuwadhalilisha wazazi wao kwa kuwakata majina.

Jina *Bimdogo* linatumika kwa ajili ya kumuita mtoto aliyezaliwa jina la bibi yake mdogo ambapo jina *Bimkuwa* linatumika kwa ajili ya kuitwa mtoto jina la bibi yake aliyemzaa mama yake. Hivyo basi, ni wazi kuwa majina hayo yanatumika kwa ajili ya watoto wa kike pekee. Ama kuhusu majina *Mbwana* na *Shaibu* yote kwa pamoja yanatumika kuwaita watoto waliozaliwa majina ya babu zao ambapo, yanatumika kuwaita watoto wa kiume pekee.

Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotumika kwa Ajili ya Kumtweza Mtu

Tukiachia majina ya asili yanayotumika kwa ajili ya kumkweza mtu, yapo majina katika jamii ya Wapemba ambayo yanatumika kwa ajili ya kumtweza mtu. Neno kutweza linatokana na neno la Kiswahili tweza⁶ kama linavyofanuliwa kwenye tini wayo hapo chini. Tangalie mifano kutoka katika Jedwali Jedwali Na. 6 lifuatalo:

Jedwali Na. 6: Majina ya Asili yenye Maana Fiche Yanayotumika kwa Ajili ya Kumtweza Mtu

Na.	Jina	Maana katika Kiswahili Sanifu
1.	Dude	Dubwana, nyangarika, hutumika kuitia kitu au mtu anayemdharau au asiyetaka kumwita jina ⁷ .
2.	Kibie	Jina linalotokana na chakula bie liloliwa wakati wa njaa kali mwaka 1972 (udogoshi)
3.	Kiembe	Jina linsalotokana na tunda embe (udogoshaji)
4.	Kikoo	Jina linalotokana na neno ukoo (uchafu) kwa lahaja ya Kipemba
5.	Kisheli	Jina linalotokana na tunda shelisheli (udogoshaji)
6.	Mchafu	Mtu asiyekuwa safi

Chanzo: Data ya Uwandani (2023)

Katika mifano iliyomo katika Jedwali Na. 6 yanajidhihirisha kwamba yamelenga kuakisi utwezaji udunishaji au udogoshaji. Kwa mujibu ya watoataarifa, majina haya, mara nyingi yalitokana na msimu wa matunda pamoja na hali ya mtoto aliyezaliwa. Majina *Kibie*, *Kiembe* na *Kisheli* walipewa watoto waliozaliwa katika msimu wa matunda hayo. Vilevile kwa kuwa, watoto hao waliozaliwa walikuwa wadogo sana majina yao yalitwezwa kwa kupewa kiambishi ya udogoshaji *ki*. Ama kuhusu majina *Dude* na *Kikoo*, tulielezwa kwamba yalitokana hali za wazazi wao walivyokuwa. Kwa mfano: *Dude* aliitwa mtoto ambaye baba yake hakuwa na msaada wowote kwenye familia yake pia alimuacha au kumtelekeza mke wake akiwa na ujauzito. Hivyo, mtoto aliyezaliwa katika mazingira hayo mama mzazi au wazazi wake walimwita mtoto huyo *Dude*. Hali kadhalika jina *Kikoo* tulielewa kwamba, aliitwa mtoto ambaye mama yake alikuwa mkoo (mchafu) hapendi kuoga au kufua na alipozaliwa alikuwa mdogo mno. Jina hilo huwa linatolewa na baba mzazi au wazazi wake.

Katika hali kama hiyo, mara kadhaa ilijitokeza sintofahamu miongoni mwa jamii hizo. Hali hiyo iliibuka kwa sababu kulikuwa na mvutano wa pande mbili kuhusu majina waliyopewa watoto hao. Matokeo yake baadhi ya watoto hao walipewa majina mengine ya ziada tofauti na yale waliyopewa hapo awali. Hata hivyo, majina waliyopewa watoto hao mara tu walipozaliwa ndiyo yalioonekana kuvuma na kutumika zaidi. Tatizo jingine linaloweza kujitokeza ni pale mtoto anapofikia umri wa kwenda shule. Mara nyingine jina lake alilopewa hapo awali linaweza kubadilishwa endapo cheti chake cha kuzaliwa limeandikwa jina alilopewa mara ya pili. Kujumla jina *Dude* linatumika kwa

⁶ Vunja heshima, beza, dharau, puuza, beua, fedhehi. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004: 410)

⁷ Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004: 68)

mtoto wa kiume wakati majina *Kibie, Kiembe, Kikoo, Kiseli* na *Mchafu* yanatumika kwa watoto wa kike pekee.

Majina ya Asili yenye Maana Fiche yanayotokana na Siku za Wiki au Idadi katika Kuzaliwa
Katika jamii ya Wapemba yapo majina wanayopewa watoto kutokana na siku walizozaliwa. Madai kama haya ya kuwapa watoto majina kwa kulingana na siku waliyozaliwa yaliwahi kuungwa mkono na Rubanza (2000) alipofanya utafiti wa majina ya watu katika kabila la Wahaya na Wayoruba. Alichunguza ubunifu wa kiisimu uliomo na alieleza kuwa majina aghalabu yanazingatia mazingira ya kuzaliwa kwa mtoto, mfuatano wao katika kuzaliwa na migongano katika jamii na muundo wa familia. Matokeo ya utafiti wake yanaonyesha kuwa majina ya watu yanabeba ujumbe unaokubalika na jamii. Aidha, mara nyingine watoto walipewa majina kulingana na idadi yao katika kuzaliwa kwao. Tuzingatie mifano katika Jedwali Na. 7 hapo chini.

Jedwali Na. 7: Majina ya Asili yenye Maana Fiche yanayotokana na Siku za Wiki au Idadi katika Kuzaliwa

Na.	Jina	Maana katika Kiswahili Sanifu
1.	Jumanne	Siku moja wapo katika wiki inayoitwa Jumanne
2.	Mosi	Namba moja mwanzo wa kuhesabu namba
3.	Pili	Namba mbili katika kuhesabu namba
4.	Tano	Namba tano katika kuhesabu namba
5.	Tatu	Namba tatu katika kuhesabu namba
6.	Wahida	Neno lenye maana ya namba moja jinsia ya kike, asili yake ni kutoka lugha ya Kiarabu
7.	Wahidi	Neno lenye maana ya namba ya moja jinsia ya kiume, asili yake ni kutoka lugha ya Kiarabu

Chanzo: Data ya Uwandani (2023)

Majina hayo kama yanavyojibainisha katika Jedwali Na. 7 hapo juu yanatokana na siku ambayo mtoto alizaliwa. au idadi ya mtoto katika familia yao. Kwa mfano: *Jumanne, Mosi, Pili, Tano* na *Tatu*. *Jumanne* na *Tano* ni majina yanayotumika kwa ajili ya watoto wa kiume peke wakati *Pili* na *Tatu* ni majina wanayopewa watoto wa kike. Aidha, jina *Mosi* anapewa mtoto aliyezaliwa siku ya Jumamosi au mtoto wa kwanza katika familia. Jina hili linatumika kwa watoto wa jinsia zote mbili yaani wanawake na wanaume. Vilevile, majina *Wahida* na *Wahidi* yanaweza kutumika zaidi kwa mtoto aliyezaliwa wa kwanza katika familia hiyo. Jina *Wahida* linatumika kwa ajili ya mtoto wa kike wakati jina *Wahidi* linatumika kwa watoto wa kiume. Hata hivyo inafaa kuisitiza hapa kwamba, majina yote hayo mara nyingine yanatolewa kinasibu tu. Inaweza ikatokea watoto wakapewa majina kama hayo bila kuwa sifa kama zilizobainishwa.

Hitimisho na Mapendekezo

Makala haya yamejikita kuchunguza majina ya asili yenye maana fiche na jinsi yanavyochanua maana katika lugha ya Kiswahili za semi zake. Uchunguzi wetu umebainisha kwamba aghalabu majina ya asili wanayopewa watu yanabeba maana mbalimbali. Katika baadhi ya majina hayo ya asili maana zake zinaakisi moja kwa moja semi kadhaa zinazotumiwa katika lugha ya Kiswahili. Ingawa kuna baadhi ya majina ambayo ni ya asli ambayo hayana uhusiano wa wazi na methali za Kiswahili. Hivyo, kwa ujumla tumegundua majina ya asili mbalimbali ambayo yana maana fiche katika Lugha ya Kiswahili. Majina hayo tumeyagawa kama ifuatavyo: Katika jamii ya Wapemba kuna majina ya asili yenye maana fiche yanayotokana na mafumbo, majina yanayotokana na maombi, majina yanayotokana na matukio, majina yanayotokana na uvumilivu. Pia, kuna majina yanayotolewa kwa ajili ya kumkweza au kmtweza mtu, majina mengine yanatolewa kulingana na siku aliyojaliwa mtoto au idadi ya mtoto katika baadhi ya familia.

Aidha, tumbainisha maana mbalimbali zinazopatikana katika lugha ya Kiswahili na semi zake pamoja na sababu mbalimbali zinazosababisha baadhi ya watu wa Pemba kuwapa watoto wao majina hayo ya kiasili. Baadhi ya sababu zilizotolewa zinaweza kuwa ni: Mateso na matatizo mbalimbali wanayokumbana nayo wanajamii, mambo mabalimbali yanayotokea katika jamii, kutaka kumpa heshima au kumdhalilisha mtu na sababu nyinginezo. Hata hivyo kwa mujibu wa watoataarifa, walidai kuwa baadhi ya majina ya kiasili kwa sasa yamepungua kwa kiasi kikubwa katika jamii. Watu wengi wanapenda kuwapa watoto wao majina wanayoyaita mazuri, mengi yakiwa yenye asili na lugha ya Kiarabu.

Tulipohoji sababu zinazowafanya baadhi ya watu kuyaacha majina yao ya asili na badala yake, kuwaita watoto wao majina yenye asili ya lugha ya Kiarabu, baadhi ya watoataarifa walitoa sababu zifuatazo: Mosi wanajamii walio wengi wanadharau tamaduni zao na kutamani kuiga mambo ya kigeni, jambo hilo limeathiri kila kitu mpaka majina ya watoto wao. Pili, baadhi ya watu wanayaona majina yao ya kiasili kama yamepitwa na wakati wanataka kwenda na usasa. Tatu, jamii wa Wapemba wengi kwa wakati huu wanasoma sana dini hivyo, wanatumia sana majina yaliyoelezwa kwenye Kur-ani tukufu na vitabu vingine vya dini. Watu wengi wanawaita watoto wao majina yenye maana katika dini ya Kiislamu na majina mengine mengi ya Mitume, Maswahaba na watu wengine mashuhuri waliofanya mambo mazuri katika Uislamu. Hivyo, ndiyo maana majina mengi ya asili kwa sasa hayatumiki kwa kiwango kikubwa kama ilivyokuwa hapo zamani.

Kwa ujumla utafiti huu ulichunguza majina ya asili yenye maana fiche ambapo kama tulivyokwisha kusema hapo kabla kwamba, majina hayo kwa kiasi kikubwa yanaelekea kupotea kutokana na baadhi ya sababu tulizokwisha kuzibainisha. Rai hii ya kufanya utafiti kama huo, iliwhi kupendekezwa na Ali hapo kabla kama asemavyo:

Tafiti zaidi za majina ya watu wa Pemba zifanywe na tafiti hizo zihusishe majina ya asili ya wapemba kwani asilimia 80 ya majina hayo yanaelekea kutpote Ali (2016: 80).

Hivyo tafiti nyingine fuatizi zinaweza kufanywa na kuchunguza tofauti za kiumbo kati ya majina yenye asili ya Kibantu na yale yenye asili ya Kiarabu. Aidha, eneo jingine muhimu ambalo linapaswa kushughulikiwa ni mchakato wa utohozi wa majina kutoka lugha ya Kiarabu unavyopokelewa katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu majina mengi ya ambayo Wapemba wanawapa watoto wao, kwa sasa yanaegemea zaidi kutoka katika lugha ya Kiarabu. Sanjari na tfiti hizo, utafiti mwingine wa uga huu unahitajika ambao utahusu chanzo na maana za majina ya maeneo mbalimbali ya Pemba.

Marejeleo

- Adam, J. and Kamuzora, F. (2008). *Research Methods for Business and Social Studies*. Morogoro: Mzumbe Book Project.
- Agyekum, K. (2006). The Sociolinguistics of Akan Personal Names. *International Journal of Humanities and Social Science*, Vol. 15(2): 206–235.
- Baitan, B. (2010). *Morphosemantic Analysis of Rubaya Person Names*. Unpublished M. A. Dissertation, University of Dar-es-salaam, Tanzania.
- Bakiza (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Braver, H. (1979). *Chinese Family and Kinship*. New York: Columbia University Press.
- Buberwa, A. (2010). *Investigating of Sociolinguistic Aspects of Place Names in Rubaya in North-West Tanzania*. Unpublished M. A. Dissertation, University of Dar-es-Salaam, Tanzania.
- Chulk, O. (1992). *Names from African: Their Origin, Meaning and Pronunciation*. Chicaco: John Benjamin Publishing.
- Bakiza (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Baitan, B. (2010). *Morphosemantic Analysis of Rubaya Person Names*. Unpublished M.A. Dissertation, University of Dar-es-salaam, Tanzania.
- Buberwa, A. (2010). *Investigating of Sociolinguistic Aspects of Place Names in Rubaya in North-West Tanzania*. Unpublished M. A. Dissertation, University of Dar-es-Salaam, Tanzania.

- Manyasa, J. (2008). *Investigating the Basis of Naming People in Kisukuma*. Unpublished. M. A. Dessertation, University of Dar-es-Salaam, Tanzania.
- Msanjila, Y. P., Kihore, Y. M. na Massamba, D. P. (2010). *Isimu Jamii Sekondari na Vyu*. Dar- Dar-es-Salaam, Tanzania
- Omary, C. and Richards, I. A. (1966). "Person Names in Social-cultural Context". *Journal of the Institute of Swahili Research, Vol. 2* (40), sep, 1970, Dar-es-Salaam Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam, Tanzania.
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.